# MSICHANA MJINGA!

***Bro. Elihuruma Maruma***

**MSICHANA MJINGA @2020**
**Elihuruma Maruma**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuhifadhi, kuchapisha kwa njia ya kielektroniki au mekaniki, kutoa vivuli, kurekodi au kubadili sehemu yeyote ya kitabu hiki kwa njia, namna na mfumo wowote bila idhini ya maandishi kutoka kwa mchapishaji.

**SIMU**: +255 752/ 715 307 008
**Facebook**: *Elihuruma Maruma*
**Instagram**: *@bro.elly247*
**Email**: *ellyrealspeaker@gmail.com*

**ISBN:**

Kimepigwa chapa na:
**CLIMAX SOLUTIONS - ARUSHA**
**+255 658 288 054 / +255 687 699 862**
***climaxsolutions8@gmail.com***

*Kurasa zimesanifiwa na Climax Solutions*

# YALIYOMO

**WAKFU;** ........................................................ vi

**SHUKRANI;** ................................................. vii

**DIBAJI;**...................................................... viii

**TAFAKURI;** ................................................. xii

**HATAKI WALA HAPENDI KUJIFUNZA** .1

**ANAJENGA MCHANGANI BADALA YA MWAMBANI!** .............................................7

**ANAAMINI HISIA KULIKO UHALISIA!** ..............................................................11

**HAJUI WALA HAJALI CHOCHOTE KUHUSU KESHO YAKE!**.........................16

**ANAHANGAIKA NA MUONEKANO WA NJE KULIKO TABIA!**..............................20

**HAJUI  KUWA MUDA HAUMSUBIRI!** ..24

**ANADHANI KUWA MSICHANA NI KUWA DHAIFU**........................................29

**ANASHINDANA NA ASILI YAKE, ANATAKA KUWA MWANAUME!** .........34

**ANAPENDA MITEREMKO, HAPENDI UTAMU WA JASHO!**.................................39

**ANANG'ANG'ANIA KUKIMBIZANA NA MITINDO NA UMAARUFU!** ....................44

**MPAKA LEO HAJUI KWAMBA SHULE SIO LAZIMA KUAJIRIWA.** ......................48

**ANADHANI WAZAZI WAMEPITWA NA WAKATI !** ...............................................52

**ANAAMINI ZAWADI NA MAWASILIANO NDIO ISHARA TOSHELEVU YA UPENDO.**......................58

**HAJUI HARUSI NI TUKIO NA NDOA NI AGANO.**................................................62

**HAJUI MWANAUME NI KAMA MICROWAVE!** ..........................................66

**HAJUI KWA MWANAUME NGONO NA UPENDO HAVIHUSIANI.**........................71

**ANAAMINI HAWEZI KUISHI BILA MTU FULANI.** ....................................................75

**OMBA NA MIMI MAOMBI HAYA;** ........79

# WAKFU;

Ninaweka Wakfu kitabu hiki muhimu kwa Mabinti, kwa Umaalumu na Umahususi kwa Binti yangu na Mwanangu Kipenzi **Darlene Elihuruma Maruma**.

# SHUKRANI;

- *Namshukuru Mungu-Baba katika Jina la Yesu kwa Uwezesho wa Roho Mtakatifu katika Uandishi wa Kitabu hiki.*
- *Naishukuru Familia yangu kwa kuwa nami katika Utumishi huu.*
- *Nawashukuru Viongozi wenzangu wa YOL Katibu Mkuu Ambwene Nkwera na Mhazini Esuvath Mollel kwa kuwa nami katika kufanikisha kazi hii.*
- *Nawashukuru Mabinti wote walionipa shuhuda na shukrani na kunitia moyo wa kuandika tena.*

# DIBAJI;

Maisha yangu hapo nyuma hayakuwa mazuri, maana yalikosa ushuhuda na hayakuwa na uhalisia wa MUNGU ndani yake. Ni kwa sababu nilifanya mambo mengi ya kijinga, na yote hayo yalitokea sio kwa kupenda ila ni kwa sababu nilikuwa na ujinga mwingi. Yaani sikuwa nafahamu vitu vingi vya muhimu, na nilikosa mafundisho mengi sahihi kuhusu maisha.

Nilikuwa msichana mjinga kwa sababu nilifanya mambo mengi nisiyo na uelewa nayo, na mengi pia sikufahamu madhara yake, na hayo yote yalinipelekea kufanya uovu mwingi ulioniumiza sana.

Mengi niliyoyafanya yalitokana na sababu kwamba nilijali hisia zaidi bila kujua uhalisia uliopo kwa maisha yangu ya baadae. Nilijikuta napelekwa na upepo, na kufanya kila litakalokuja mbele yangu au kwenye akili yangu bila hata kufikiri au kutaka ushauri, lakini baada ya hapo nilijuta sana na mnoo!.

Nilishindwa kujali kesho yangu, zaidi sana nilishindwa hata kujua na kujali thamani ya usichana wangu, na ndio sababu kubwa ya mambo yote yaliyofanyika.

Wasichana wengi sana hawatambui thamani ambayo MUNGU ameweka ndani yao, bali wanaishia kupenda na kujali visivyofaa tena vya muda mfupi, na baadae kupoteza kabisa mwelekeo. Wasichana wengi siku hizi tunajali pesa na tunasukumwa na ushabiki na hisia pia, ndio

maana tunashindwa kuepuka kufanya mambo mabaya ambayo kwa namna moja au nyingine yanatupoteza.

Kitabu hiki cha “Msichana Mjinga” kimeeleza wazi uhalisia wa msichana mjinga kama ilivyokuwa kwangu, lakini pia kimetoa mafunzo na maarifa zaidi ya kumbadilisha msichana mjinga. Lengo kuu ni kumuonyesha na kumrejeshea thamani yake na kumsogeza karibu na MUNGU, kwani kimejumuisha mafundisho yatokanayo na Neno la Mungu.

Nikualike msichana mwenzangu uliyepo shuleni, chuoni, mtaani hata kazini katika kukisoma kitabu hiki kizuri kitakachokupa maarifa ya kutosha na kuondoa ujinga ulioko akilini, na hatimaye urudishe ile thamani yako iliyopotea na uondoe ule ukale

uliokuwa ukiishi ndani yako kupitia mafundisho na Nguvu ya Neno la Mungu.

Nikutakie shule njema, bila kusahau kumuomba Roho Mtakatifu akusaidie katika kuelewa mafundisho yote na akupe Mabadiliko na Urejesho katika Jina la Yesu!, **AMEN!.**

**Ms Esuvath Richard Mollel.**

**Machi, 2020**

# TAFAKURI;

***" Maana katika dirisha la nyumba yangu Nalichungulia katika shubaka yake; Nikaona katikati ya wajinga, Nikamtambua miongoni mwa vijana, Kijana mmoja asiyekuwa na akili, …"*** Mithali 7:6,7.

Unajua bhana hili jambo lililomtokea Suleimani, lilinitokea na mimi pia, sema tofauti yetu ni kwamba yeye aliona kupitia dirisha la nyumba yake ILA mimi nimeona kupitia uzoefu wa maisha niliyoishi. Yeye alimuona kijana wa kiume, ILA mimi nimemuona msichana. Na huyu msichana niliyemuona mimi nilionelea jina litakalomfaa vizuri na kumtoshea ni MSICHANA MJINGA.

Msichana Mjinga sio jina baya sana kama unavyofikiria, Ujinga ni kutojua jambo/ mambo/ kitu fulani hasa unachopaswa kujua. Mtu huwa mjinga kwa yale asiyoyafahamu au kutokuwa na uelewa nayo.

Huyu Binti au Msichana niliyemuona mimi na hasa kwa yale aliyokuwa anayafanya na vile alivyokuwa anaenenda, niligundua kwa haraka kwamba kuna mambo mengi alikuwa hayafahamu au hana uelewa nayo, na hii ndiyo sababu alikuwa anafanya alichokifanya bila kujali.

***“Pokea mafundisho yangu, wala si fedha, Na maarifa kuliko dhahabu safi. Maana hekima ni bora kuliko marijani; Wala vyote vinavyotamanika havilingani nayo.”*** Mithali 8:10,11.

Basi na Mimi nikadhamiria kwamba nisiishie kumuona tu na kuumia, badala yake nikanuia nimuite nimuweke chini, na kisha nimuonyeshe UJINGA wake, pamoja na kumpa ufahamu utakao msaidia kuondokana na huo UJINGA.

Msichana Mjinga niliyemuona mimi alikuwa mmoja tu ILA najua anawakilisha au anatoa taswira halisi ya mamia kwa maelfu ya mabinti wengi ambao UJINGA umekuwa ukiwagharimu, ukiwatesa, ukiwahuzunisha na hata kuwarudisha nyuma. Wasichana wengi kwa kukosa hekima na ufahamu sahihi wamekuwa wakiishi maisha ya kubahatisha na kupapasapapasa, na wamekuwa wakijigonga na kuambulia maumivu makali.

Huyu Msichana Mjinga mmoja niliyemuona Mimi nilipata nafasi ya kuketi nae na

kuyajenga kwa kina, na kwa kweli baada ya mazungumzo yetu maisha yake yamebadilika kabisa kabisa. Na kwa sababu ni ngumu kuketi na kila msichana mjinga, Mimi kaka yenu nikasema nizungumze na ninyi kupitia maandishi haya murua.

Kuna tabia nyingi nimeziandika ndani ya kitabu hiki zinazoonyesha UJINGA katika namna mbalimbali, ikiwa kuna namna aidha moja au mbili ambazo umekuwa ukiishi hivyo pia ,basi na wewe ni MSICHANA MJINGA katika hilo. Unachopaswa kufanya ni kukubali ujinga wako, na kuamua kufuata kanuni za mabadiliko zilizoainishwa ndani ya kitabu hiki ili uondokane na huo ujinga.

***" Enyi wajinga, acheni ujinga, mkaishi, Mkaende katika njia ya ufahamu."*** Mithali 9:6

# MWANAMKE MJINGA

# HATAKI WALA HAPENDI KUJIFUNZA

1 Wakorintho 8:2 ***“Mtu akidhani ya kuwa anajua neno, hajui neno lo lote bado, kama impasavyo kujua.”***

Warumi 1:22 ***“Ingawa wakijidai kuwa wenye hekima, wakawa wajinga.”***

Msichana Mjinga ni yule ambaye hapendi wala hataki kujifunza. Huwa anadhani tayari anajua kila kitu. Hana kabisa muda wa kujifunza na kudadisi masuala mbalimbali yanayomuhusu. Na hata ikitokea unajaribu kumueleza juu ya jambo fulani ambalo unaona kabisa kwamba halijui na litamgharimu, bado ataonyesha kudharau ama kutokukusikiliza kabisa.

Nguvu ya mtu kuzishinda changamoto za kila siku maishani ni MAARIFA. Mtu mwenye maarifa ni mtu asiyezuilika na asiyewezwa kwa urahisi. Unapojua UKWELI au UHALISIA juu ya jambo fulani, hilo jambo kamwe haliwezi kukusumbua. Wasichana wengi wanaumizwa na kuteseka kila leo, kwa sababu tu hawajui uhalisia na ukweli wa mambo. UJINGA umewagharimu wasichana wengi kwa sababu ni wazito sana kwenye kujifunza. Unapoleta majivuno na kufikiri kwamba unajua kila kitu, na kudhani kwamba uko sahihi kwenye kila kitu, utaangukia pua na kuishia maumivu, majuto na mateso.

Mithali 22:3 ***"Mwenye busara huyaona mabaya na kujificha, Bali wajinga huendelea mbele wakaumia."***

***“Mtu mwenye busara huona hatari na kukimbia, bali mjinga huendelea mbele kama kipofu na kuteswa nayo.”***

Ni muhimu sana kwako kama msichana uamue kujenga tabia ya kujifunza juu ya mambo mbalimbali yanayohusu maisha yako. Hakikisha kabla haujajiingiza kwenye chochote uwe umepata muda wa kutosha kujifunza juu ya hilo jambo. Kwa mfano kabla hujajiingiza kwenye mahusiano ya kimapenzi hakikisha una maarifa ya kutosha juu ya hilo eneo, kabla haujaanza biashara jifunze kuhusu biashara, kabla hujaamua kufanya jambo fulani hakikisha una maarifa ya kutosha juu ya jambo hilo.

Zipo njia nyingi mno za kukusaidia uondokane na ujinga kwa kujifunza yakupasayo. Mfano njia rahisi ni kwa KUWAULIZA waliokutangulia kwenye

hilo eneo na wakafanikiwa. Haitakupunguzia chochote unapouliza zaidi sana itakuongezea, hata Waswahili waliwahi kusema KUULIZA SIO UJINGA.

Mithali 1:4,5 ***“Kuwapa wajinga werevu, na kijana maarifa na hadhari; mwenye hekima asikie na kuongezewa elimu, na mwenye ufahamu ayafikie mashauri yenye njia.”***

Anza kujenga tabia ya KUSOMA VITABU sahihi kuhusiana na mambo mbalimbali ya maisha yako. Wekeza muda wa kutosha kujifunza MAANDIKO MATAKATIFU yaani BIBLIA, hakuna kitabu bora duniani kitakachokuvusha kwa uhakika kama hiki. Nunua na soma vitabu mbalimbali kuhusu biashara, mahusiano, fedha, afya, na nyanja mbalimbali za maisha.

Mithali 4:7 ***“Bora hekima, basi jipatie hekima; Naam, kwa mapato yako yote jipatie ufahamu.”***

Siku zote maarifa ni gharama, kuanzia fedha, muda na mengineyo. Pia jenga tabia ya kuhudhuria semina, makongamano, warsha na mikutano mbalimbali itakayokusaidia kupata maarifa ya kutosha juu ya mambo mbalimbali. Usisahau pia kwamba unaweza kujifunza kupitia mitandao mbalimbali mfano Youtube na nyinginezo.

Msichana mwenye MAARIFA ni Msichana mwenye Nguvu ya kuzishinda Changamoto, vikwazo na vizuizi mbalimbali. Na kamwe usisahau kwamba kuwa na MAARIFA tu haitoshi bali kuyaweka MAARIFA katika vitendo ndiko kunakokupa nguvu ya kutosha.

Nakuombea uondokane na hali ya kutopenda kujifunza, wasichana wengi wamedanganyika na kuumia kirahisi kwa sababu tu hawakutaka kujifunza, na ujinga wao uliwagharimu. Isitokee kwako ukadhania unajua sana halafu mwisho wa siku ukaungua na jua. Biblia inasema mwenye busara (maarifa) huiona hatari akajificha, bali mjinga huendelea mbele akaumia. Kama unajua unajua, na kama hujui hujui tu. Usilete mbwembwe na maigizo mwisho wa siku ukaambulia maumivu. Nasisitiza JIFUNZE JIFUNZE JIFUNZE JIFUNZE, itakusaidia sana.

# ANAJENGA MCHANGANI BADALA YA MWAMBANI!

Uimara wa nyumba au jengo lolote ni MSINGI. Hata kama nyumba ingekuwa na muonekano mzuri kiasi gani, kama msingi wake ni mbovu au dhaifu ipo siku tu hii nyumba na uzuri wake wote ITAANGUKA na mahali pake pasionekane tena. Kadhalika na msichana ambaye amejenga maisha yake kwenye misingi mibovu, msichana ambaye ameweka tegemeo na tumaini lake kwenye muonekano, elimu na watu flani flani. BIBLIA inatufundisha hivi;

Mathayo 7: 24 – 27 ***“Basi kila asikiaye maneno yangu, na kuyafanya,***

***atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke, kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba. Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa."***

Msichana mjinga hana tofauti sana na huyo bwana ambaye alijenga nyumba yake mchangani, na yalipomkuta makubwa akaanguka na tena anguko lake likawa kubwa. Nikuulize swali rahisi tu NI NANI/ NINI NDIO MSINGI/ TEGEMEO LA MAISHA YAKO? NI NINI/ NANI NDIO

HASA HAKIKISHO LA MAISHA YAKO?.

Majibu ya haya maswali ndiyo yatanisaidia kujua kama wewe ni Msichana Mjinga au la! Biblia inasema hivi ***"Na dunia inapita pamoja na tamaa zake, bali ayafanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele."*** Ikiwa umeweka tumaini lako ama ikiwa umejenga msingi wako juu ya watu au vitu ni wazi hauna tofauti na huyu bwana aliyejenga mchangani.

Nisikilize kwa umakini sana, Msichana asiye mjinga namfananisha kwa 100% na huyu bwana aliyejenga juu ya Mwamba. Ni msichana anayejua na kutambua kwamba chanzo/ msingi/ asili ya uhai/ maisha/ uzima wake ni Mungu Baba katika Jina la Yesu. Na kwa hiyo ameyatoa/ ameyakabidhi/ ameyaunganisha maisha yake na Mungu, na

anachokifanya ni kumpenda, kumtii na kumheshimu Mungu kwa kila hatua ya maisha yake sawasawa na NENO LA MUNGU.

Na hii ndio sababu hata anapopitia changamoto na vishawishi mbalimbali vya maisha na ujana, bado hawezi kutetereka kwa sababu amejenga juu ya mwamba.

Nakushauri leo, Chagua kujenga juu ya Mwamba ambapo ndipo penye uhakika wa maisha yako ya sasa na ya baadae. Nakuhakikishia hautajutia uamuzi huu ambao utabadili kabisa uelekeo wa maisha yako. Hongera kwa KUOKOKA.

# ANAAMINI HISIA KULIKO UHALISIA!

Wasichana daima huongozwa/ huendeshwa kwa HISIA. Hii ni ASILI yao. Mara nyingi chochote kinachokuja mbele yao hukikabili kwanza kwa HISIA. Hata na hivyo HISIA sio mbaya, japo kuamini kila HISIA ndio mbaya. Msichana Mjinga ni yule anayeamini kila HISIA hata kama anaona kabisa kuna UHALISIA katika hilo jambo. Mara nyingi hata kama kitu kilianzia kwenye HISIA, kwa kadri muda unavyozidi kwenda lazima kuna viashiria vitaanza

kuonekana juu ya UHALISIA wa zile HISIA.

Ni vizuri uelewe kwamba sio kila HISIA uliyonayo inaweza kuwa halisi au sahihi. Mimi nimeona mabinti wengi wakiumia kwa sababu tu waliziamini na kufuata HISIA zao, wakijidanganya wanafuata mioyo yao.

Mithali 18:13 ***“Yeye ajibuye kabla hajasikia, Ni upumbavu na aibu kwake.”***

Ni wazi kama msichana kila wakati atakuwa na HISIA, lakini nikutahadharishe kwamba JIPE MUDA kabla ya kuamini hizo HISIA. Nimewaona wengi ambao walikutana na WAVULANA kwenye mazingira flani flani, na hiyo ikawafanya kwa HISIA zao wawaamini kwa ghafla, na wakaingia nao kwenye mahusiano na matokeo yake

wakaishia MAUMIVU makali. Wapo waliowaamini watu kwa ghafla kwenye biashara na mwisho wa siku wakaambulia HASARA. Wapo waliojenga urafiki na watu kwa ghafla bila kuwafahamu vizuri, baada ya muda mchache wakavuna USALITI.

Achana kabisa na dhana za kuamini mara MOYO au HISIA zako kwa haraka, UAMINIFU unapimwa na unajengwa na MUDA. Kuhisi tu hakutoshi kutoa majibu ya mwisho wa usahihi wa jambo. Na ndio maana wataalamu wanashauri pia kwamba ukiwa na furaha sana USITOE AHADI, na ukiwa na huzuni au hasira sana USIFANYE MAAMUZI. Hisia zina ladha ya pekee kwenye nafsi ya mtu, ila ukiziruhusu zikuendeshe au zikutawale utapata MAUMIVU, MAJUTO, HASARA na

LAWAMA kila wakati. Narudia tena na tena JIPE MUDA!

Hizi mambo za kuwa na HISIA KALI mpaka uache AKILI, na wengine hata kumuomba Mungu hamuamini tena ni hatari sana. Mambo ya kudumu na yenye thamani hayajengwi kirahisi.

*“Naamini ni Mwanaume anayenifaa, anaonekana ni HUSBAND MATERIAL, Naamini hii biashara ina faida sana, Naamini kwa anavyoonekana ni rafiki mzuri. Nilivyomuona tu moyo wangu ukaniambia huyu ni MUMEO. Unajua ni Mtumishi wa Mungu hawezi kuwa kama wanaume wengine. Ujue anafahamiana na kakaangu na wanasali wote, hawezi kunirusha n.k n.k n.k”*

ACHANA NA HISIA, JIPE MUDA ili upate UHALISIA.

HISIA zinaweza kukupa RAHA, kumbe UHALISIA wake ni KARAHA.

# HAJUI WALA HAJALI CHOCHOTE KUHUSU KESHO YAKE!

Msichana mjinga anaona mwisho wa pua yake na si zaidi ya hapo. Huwa anaitumikia siku tu baada ya hapo hana cha kupoteza. Akishaamka, akafanya usafi, akaoga, akavaa, akajipodoa, akajua anakula nini, na akawa na kifurushi cha data kwa simu yake NA ana muvie au series ya kuangalia, SIKU IMEISHA.

Yaani hawazi chochote kuhusu kesho yake, na haimsumbui sana kuhusu maisha yake ya baadae. Kwake kila kitu ni SAWA. Msichana Mjinga hana TASWIRA wala PICHA yoyote juu ya maisha yake ya

baadae. Na ndio maana anaweza kufanya jambo lolote wakati wowote bila kujali chochote. Kwenye akili na fikra zake hajui kwamba kila LEO inajenga KESHO.

Ikiwa hauna NDOTO, MAONO, MALENGO au MIPANGO juu ya maisha yako ya baadae kuanzia mwaka 1, miaka 3, miaka 5 na kuendelea, anza kujitazama kama Msichana Mjinga na asiyejielewa. Maandiko Matakatifu yanasema hivi;

Mithali 29:18 ***"Pasipo maono, watu huacha kujizuia; Bali ana heri mtu yule aishikaye sheria."***

Ukiona msichana anaishi maisha ya sukuma siku, na kujiachia bila nidhamu na adabu, elewa moja kwa moja kwamba huyo msichana hajui wala hajali kuhusu kesho yake. Kwa mtu yeyote anayejali KESHO/

UBAADAE wake, ni lazima awe na NIDHAMU ya namna anavyoitumia LEO yake. Na daima hujiwekea MIPAKA na MISIMAMO juu ya nini afanye na nini asifanye. Na ukitaka kujua kesho ya mtu itakuwaje, angalia kwa umakini namna anavyoitumia leo yake.

Msichana ambaye hajajiwekea Malengo wala vipaumbele, tena asiye na NDOTO wala shauku ya kufika mahali flani na kuwa mtu fulani, ni aina ya msichana anayeweza kufanywa chochote mahali popote MAANA hana sababu ya kujizuia wala kujidhibiti.

Msichana asiyeanza kujiona LEO mke wa mtu mwenye heshima NA mama wa watoto mwenye nidhamu, tena mwanamke wa mfano kwenye jamii, kamwe huyu msichana hawezi kujizuia. Na ikumbukwe tu kwamba KILA tunachokipanda leo ni dhahiri

kwamba tutakivuna kesho. Msichana ukipanda uvivu, uzembe na kutojali utavuna UMASIKINI, lakini pia ukipanda ufuska na uasherati utavuna Mimba, UKIMWI na aibu pale baadae.

Usichana unapita, Urembo unapita, Uzuri unaisha, na siku na miaka inakwenda. Amka toka usingizini, Shtuka na Chukua hatua. Wewe ndio mchoraji pekee wa ramani ya hatma ya maisha yako, Chora ile Ndoto kubwa na nzuri. Iwekee malengo, mikakati na mipango ya kuifikia. Na anza kuitumia leo vizuri kwa ajili ya hiyo kesho yako njema. Ninaamini umenielewa vizuri msichana, Usije kusema SIKUAMBIWA!.

# ANAHANGAIKA NA MUONEKANO WA NJE KULIKO TABIA!

Nisikilize binti, Unajua kuna vitu vya muda mfupi na kuna vitu vya kudumu. Kuna mambo ya muhimu na kuna mambo ya lazima. Wengi wa mabinti wa leo wanahangaika sana na muonekano wao wa nje, na huko ndiko wanakoekeza muda, fedha na akili zao. Yaani kila wakati mtu anawaza atavaaje, atasukaje, atapunguzaje tumbo au ataongezaje hiki au kile. Nguo gani itaendana na ile, mafuta gani yataondoa hiki au yataongeza kile. Viatu gani vitaendana na nguo ile, mshono gani utabamba zaidi. Simu gani ndio itaendana nae na ataipataje. Yote

katika yote ilimradi tu na yeye aonekane kwa namna ya nje kwamba ni wa kisasa na anapendeza. Mtume Petro kwa kuongozwa na Roho alisema hivi;

1 Petro 3:3,4 ***"Kujipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi; bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu."***

Naomba nisieleweke vibaya, sijasema usipendeze ama usionekane nadhifu, ila ikiwa utatumia muda wako wote kuyawaza na kuyahangaikia haya, basi ni wazi wewe ni Msichana Mjinga. Maisha ni zaidi ya vile watu wanavyokuona kwa namna ya nje, maisha ni zaidi ya mavazi, fasheni na mitindo.

Baadhi yenu mnaonekana mnapendeza kwa nje ILA sasa kichwani hamna kitu. Wengi wenu mnapendeza ILA tabia zenu ni mbaya zisizoelezeka. Wengi wenu mnapendeza ILA hamjui lolote kuhusu kesho yenu. Wengi wenu mnapendeza lakini hamna Mungu ndani yenu na ndio maana mnasumbuliwa na manguvu ya giza kila leo.

Hii ni habari njema kwako ambayo itakuondolea huo ujinga, MUONEKANO haudumu na utakupa mvulana wa kulala nae na kula nae maisha kwa muda mfupi ILA TABIA itakupa mume wa maisha yako yote. MUONEKANO utakupa sifa za muda mfupi ILA TABIA itakupa sifa za kudumu maisha yako yote. Na sasa ushauri wa bure ni huu hapa, badala ya kuwekeza muda ,fedha na akili kwenye MUONEKANO, wekeza

muda, fedha na akili yako kwenye kujenga na kuboresha TABIA NJEMA.

Badala ya kufikiria sana mavazi, urembo, makeups, nywele, mafuta na manukato ANZA kufikiria vile utajenga upendo, utulivu, upole, bidii, malengo, utakatifu na unyenyekevu. Nataka nikuhakikishie kwamba TABIA njema na MUONEKANO mzuri utakufanya uwe bora na wa thamani sana, ILA MUONEKANO mzuri bila TABIA njema vitakufanya uwe wa kutumika na kutupiliwa mbali.

AMUA LEO, AMUA SASA, ANZA LEO, ANZA SASA kujipamba kwa TABIA njema na maadili mema.

# HAJUI KUWA MUDA HAUMSUBIRI!

Zaburi 139:16 ***“Macho yako yaliniona kabla sijakamilika; Chuoni mwako ziliandikwa zote pia, Siku zilizoamriwa kabla hazijawa bado.”***

Ukweli ambao inawezekana hauufahamu ni SIKU ZAKO ZOTE za kuishi zilishaandikwa kitabuni mwa Mungu kabla hata haujazaliwa. Na kwa hiyo fahamu ya kwamba MAISHA yako yamepimwa kwenye MUDA. Unapochezea MUDA wako maana yake ni kwamba unachezea MAISHA yako. Ni muhimu ufahamu kwamba hautaishi milele, kama ambavyo

ulizaliwa siku moja kadhalika utakufa siku moja.

Na mabinti wengi hawafahamu kwamba Mungu aliwaleta duniani kwa kazi au kusudi maalumu, na hilo kusudi alilipa muda maalum wa kulitimiza. Muda uliopewa kuishi ndio muda haswa unapaswa kuutumia kwa KUSUDI LA MUNGU.

Mhubiri 3:1 ***"Kwa kila jambo kuna majira yake, Na wakati kwa kila kusudi chini ya mbingu."***

Mhubiri 3:11 **"*Kila kitu amekifanya kizuri kwa wakati wake;* tena ameiweka hiyo milele ndani ya mioyo yao; ila kwa jinsi mwanadamu asivyoweza kuivumbua kazi ya Mungu anayoifanya,tangu mwanzo hata mwisho."**

Fahamu kwamba huna muda wa kufanya kila kitu ILA unao muda wa kutosha kufanya yale ambayo Mungu amekuletea duniani kuyafanya. Muhimu ni kutambua wakati na majira sahihi, wa kufanya jambo sahihi kwenye eneo sahihi na kwa usahihi. Na kitu kizuri alichokifanya Mungu ni kule kufanya kila kitu kuwa kizuri na sahihi kwa wakati wake.

Wasichana wengi wajinga huwa wanadhani wana muda wa kutosha kuchezea na kufanya tu mambo wanayoyataka yasiyo na maana wala faida, pasipo kujua kwamba wanachezea maisha yao. Haitatokea hata siku moja MUDA ukakusubiri, jifunze kufanya mambo sahihi kwa wakati sahihi vinginevyo majuto ni mjukuu. Wakati wa kusoma SOMA, Wakati wa kujiandaa JIANDAE, Wakati wa kuomba OMBA,

Wakati wa kuolewa OLEWA. Komboa wakati,

Waefeso 5:16 ***"mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu."***

Maisha haya yamejaa kila aina ya vishawishi na vipoteza muda. Ni vema utambue KUSUDI, MAONO na MALENGO yako na kisha weka vipaumbele na ratiba maalumu ya kuhakikisha haupotezi muda. Muda ni rasilimali muhimu sana ambayo ukipoteza hauwezi kuirudisha, ila ukiitumia vizuri ni rahisi kufanikiwa.

Sikiliza Msichana, Acha kuchanganya mambo, Acha kupoteza muda. Tulia, Tafakari na Tumia muda wako vizuri ili Mungu akuonekanie. Niliwahi kuwaambia USIOLEWE kabla HAUJAOLEWA, kitu

chochote kikifanyika nje ya muda wake kinapoteza thamani na ubora wake. Ninakuombea utambue NYAKATI na MAJIRA Mungu aliyokupa ili ufanye kama atakavyo Yeye.

Kumbuka MUDA WAKO ni MAISHA YAKO!.

# ANADHANI KUWA MSICHANA NI KUWA DHAIFU

Waamuzi 4:14 ***“Debora akamwambia Baraka, Haya! Inuka; maana siku hii ndiyo siku ambayo BWANA amemtia Sisera katika mkono wako...''***

Debora, moja kati ya Waamuzi wa kipindi kile ambaye peke yake alikuwa ni Mwanamke. Kwenye hiki kisa tunaona Baraka (Mwanaume) akiwa na hofu na uoga kwenda kwenye haya mapigano. Lakini Debora anamtia nguvu Baraka katika BWANA kwa kumwambia kishujaa HAYA! INUKA; na haishii tu kumtia nguvu bali anakwenda pamoja naye.

Nataka ufahamu kwamba kuwa MSICHANA (Mwanamke) si kuwa dhaifu, na wala si kujiweka nyuma nyuma huku ukiwa na fikra za kwamba kwa kuwa wewe ni msichana hauwezi hiki wala kile. Ndani yako iko Nguvu ya ajabu ya kutenda mambo makubwa kwa uweza wa Mungu. Yako mambo ya kutumia akili, hekima, maarifa, ubunifu na ushawishi wako (asili) yako kama mwanamke. Hebu angalia Abigaili alivyomnusuru mumewe:-

1 Samweli 25:23 ***"Ndipo hapo Abigaili alivyomuona Daudi, alifanya haraka kushuka juu ya punda wake, akamwangukia Daudi kifulifuli, akainama mpaka nchi."***

Hapa unaona Abigaili anamuokoa mume wake NABALI (mpumbavu) pamoja na nyumba yake dhidi ya mikono ya Daudi.

Hekima na ufahamu wa huyu mwanamke ulimfanya Daudi akaghairi kwenda kumuua NABALI na nyumba yake yote. Nataka uondokane na UJINGA na uanze kuona nguvu uliyonayo kama mwanamke ya kuleta MABADILIKO na MATOKEO chanya kwenye maisha yako na wengine.

Weka mbali dhana na mtazamo potofu wa kutoweza hiki au kile, na badala yake JITIE nguvu katika BWANA na CHUKUA HATUA. Nuia kufanya jambo, na anza hilo jambo.

Angalia Mwanamke wa Mithali 31

Mithali 31: 11, 13, 16, 18, 20.

***"Moyo wa mumewe humwamini, Wala hatakosa kupata mapato. Hutafuta sufu na kitani; Hufanya kazi yake ya mikono kwa moyo. Huangalia shamba, akalinunua,***

***Kwa mapato ya mikono yake hupanda mizabibu. Huona kama bidhaa yake ina faida; Taa yake haizimiki usiku. Huwakunjulia maskini mikono yake; Naam, huwanyoshea wahitaji mikono yake."***

Huyu alikuwa mwanamke ALIYEJITAMBUA, pamoja na kuolewa hakuishia kukaa tu nyumbani bali ALIJIONGEZA. Dunia ya leo inahitaji wasichana walioamua kuachana na UJINGA na kuamua kuweka dhana potofu pembeni, na badala yake wanatumia kila ambacho Mungu ameweka ndani yao kuhakikisha kwamba wanaleta matokeo. Hebu na wewe USILALE wala USIKAE NYUMANYUMA bali kwa unyenyekevu na umakini mkubwa iendee NDOTO na ile SHAUKU iliyojaa moyoni mwako.

Kimsingi hakuna cha kukuzuia isipokuwa WEWE MWENYEWE, Inawezekana KUFANYA ZAIDI, Inawezekana kuwa MFANO WA KUIGWA, na zaidi Inawezekana kuwa KIELELEZO.

Ondoa dhana potofu ya kwamba, KUWA msichana ni kuwa DHAIFU.

# ANASHINDANA NA ASILI YAKE, ANATAKA KUWA MWANAUME!

Mungu wetu ni wa ajabu sana kiukweli, Ninapoangalia na kujifunza kwa kina kuhusu UUMBAJI, ninamshangaa sana Mungu. Yeye mwenyewe alipomaliza UUMBAJI, alitazama vyote alivyoviumba akaviona kuwa vyema na vyenye kupendeza.

Halikadhalika ukiangalia namna ya ajabu alivyomuumba Mwanaume na Mwanamke, ni viumbe vya kuvutia sana. Hebu tuangalie maandiko haya;

Mwanzo 2:18, 23 *"**BWANA Mungu akasema, Si vema huyo mtu awe peke yake,***

***nitamfanyia msaidizi wa kufananana naye. Adamu akasema, Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume."***

Mungu alijua tangu awali kabla hata hajawaumba, ya kwamba ili Dunia iwe mahali pazuri pakuishi lazima awepo mwanaume na mwanamke. Na ndio maana yeye mwenyewe akasema SI VEMA. Ni hatari na janga kubwa sana kwa mwanamke au mwanaume kukataa ASILI yake ya mwanamke au mwanaume na kutaka kulazimishia kuwa kinyume na uhalisia wake. Unachopaswa kufahamu ni kwamba ni Mungu mwenyewe alitaka na aliona inafaa kulingana na kusudi alilokuleta duniani kufanya, ya kwamba wewe uzaliwe

mwanamke. Na anasikia fahari kubwa kwa wewe kuwa mwanamke.

Jambo baya lililoingia duniani leo na linataka kuiharibu dunia, ni hili la baadhi ya wanawake kutaka kuwa wanaume. Wanaamua kuondoka kwenye misingi, asili, nafasi na majukumu ya kike na kuanza kulazimishia kuwa wanaume. Hii imekuwa chanzo na sababu ya ugomvi mkubwa kwenye NDOA na familia nyingi leo. Biblia inasema hivi;

Mithali 17:14 ***"Mwanzo wa ugomvi ni kama kutoboa penye maji; Basi acheni ugomvi kabla haujafurika."***

Kitendo cha mwanamke kutaka kumtawala mwanaume ni kuondoka kwenye asili yake, kitendo cha mwanamke kutaka kuwa msemaji na kiongozi wa juu wa familia ni

kumuondolea mwanaume uanaume. Uongozi na Utawala wa familia ni asili ya mwanaume aliyoumbiwa na Mungu mwenyewe. Maandiko yanasema enyi WAKE watiini waume zenu, hii maana yake ni kujitiisha na kujinyenyekeza chini ya mamlaka ya mwanaume. Unaweza kumshauri hata kumkosoa mwanaume sirini kwa upendo na hekima ya hali ya juu.

Leo tuna wasichana wengi wajinga wasioambilika wala kushikika, tena wenye dhamira mbaya ya kwamba hawawezi kuwa chini ya mamlaka ya mwanaume, tena hawataki kunyimwa uhuru wao.

Mithali 21:9 ***"Ni afadhali kukaa kwenye pembe ya darini, Kuliko katika nyumba pana pamoja na mwanamke mgomvi."***

Wapo wasichana ambao kwa namna tu wanavyoishi, vijana wengi wa kiume wanajiuliza ikiwa watakuwa salama baada ya kuoa aina hii ya wasichana, na wengi wanaishia kukimbiwa na kuachwa.

Ushauri wangu ni huu, maadamu Mungu amekuumba msichana hebu tulia kwenye asili na uhalisia wa mwanamke. Inavutia sana na inamtukuza Mungu ikiwa Msichana atabaki kuwa Msichana na Mvulana atabaki kuwa Mvulana. Kuna baraka, kibali na mafanikio unapokaa kwenye asili, nafasi na kusudi lako kama mwanamke. Migogoro na shida nyingi leo zinatokana na watu kukimbia kwenye asili na nafasi zao, Acha Mwanaume awe Mwanaume NA Mwanamke awe Mwanamke.

# ANAPENDA MITEREMKO, HAPENDI UTAMU WA JASHO!

Kila wakati ambao Mungu anaponipa fursa ya kuzungumza na mabinti, huwa nawaambia **"VYA BURE VINA GHARAMA kuliko VYA KULIPIA."** Ni asili ya mwanamke kupokea, ila hatakiwi kupokea kila kitu kutoka kwa kila mtu tena kila muda. Kinachowagharimu wasichana wengi wajinga mpaka kujikuta wanakuwa Watumwa wa watu, ni UVIVU na kupenda MITEREMKO.

Mithali 6:6 *"**Ewe mvivu, mwendee chungu, Zitafakari njia zake ukapate hekima.**"*

Na wanaume wengi wamekuwa wakitumia vizuri sana huu UJINGA wa Wasichana wa leo. Atakuja mwanaume atakupa kila unachotaka lakini mwisho wa siku atakutumikisha MWILI WAKO ataijeruhi NAFSI yako, na utajikuta unaambulia maumivu makali yaliyosababishwa na wewe kupenda MITEREMKO.

Ni vizuri sana ukianza kubadili namna unavyoishi, yaani mtindo wako wa maisha, jitahidi kujidhibiti uanze kuishi kulingana na uwezo na uhalisia wa maisha yako. Acha kupenda na kulazimishia kuishi maisha usiyo na uwezo nayo. TAMAA mbaya imewagharimu Wasichana wengi wajinga. Na kwa taarifa yako UTAMBULISHO wako halisi, haupo kwenye vitu unavyomiliki ama mtindo wa maisha unaouhangaikia. UTAMBULISHO wako

halisi ni vile unavyojiona na unavyojiangalia, Achana kabisa na maisha ya kuwafurahisha watu wakati moyoni unajihukumu.

Mithali 12:24 ***"Mkono wa mwenye bidii utatawala, Bali mvivu atalipishwa kodi."***

Hakuna furaha na amani toshelevu kama KUMILIKI vitu na KUISHI maisha ambayo umeyatafuta kwa jasho lako. Yaani mtoto wa kike umefanya juhudi na jitihada, kwa kufanya kazi halali kwa mikono yako mwenyewe NA ukapokea ujira halafu sasa ndio unatanua nao mjini. Umejishughulisha kwa bidii, ukajipatia faida, kisha unatumia sehemu ya faida kujinunulia simu kali, kujinunulia viwalo vya maana, umejinunulia gari lako ama umejijengea nyumba yako. Huu unaitwa UTAMU WA JASHO lako, na ladha yake ni tamu kuliko vitu vya

mteremko ambavyo unaweza kunyanyasiwa usiku na mchana na bado usipate amani navyo.

Ondokana na UJINGA wa kupokea pokea vitu ambavyo hujavitolea jasho, kama upo tayari kuthaminishwa thamani ya mwili wako na vitu vinavyopita, basi ENDELEA kupokea. Ila tambua hakuna aliyewahi kukimbia mbio kali kwenye mteremko na akabaki salama. Mungu hubariki kazi ya mikono yetu, kufanya KAZI kuna maumivu yake, ila hayo maumivu hugeuka furaha wakati wa mavuno.

Zaburi 126:5 ***"Wapandao kwa machozi Watavuna kwa kelele za furaha."***

Hii ni tofauti na wepesi unapopokea vya bure ila baadae MAUMIVU yanakuwa makali na ya kudumu wakati unavilipia.

***"NOTHING goes for NOTHING! "***

Chukua HATUA, fanya BIDII, Umiliki vya KWAKO!

# ANANG'ANG'ANIA KUKIMBIZANA NA MITINDO NA UMAARUFU!

Kila mmoja wetu ameumbwa kwa namna ya pekee, hivyo kila mmoja ni wa pekee. Dunia ina watu zaidi ya Bilioni 7 ila hakuna wa kufanana na wewe. Na alichokuleta Mungu kufanya duniani ni wewe peke yako unaweza kufanya, na ndio maana aliruhusu uzaliwe, na amekulinda mpaka leo unaishi. Hivyo hauna sababu yoyote ya kujilinganisha au kujifananisha na mtu yeyote hata kama mmezaliwa nae mapacha, sikiliza;

Wafilipi 2:3 ***"Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa***

***unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake.*** "

Dunia tunayoishi leo imejaa mambo lukuki mapya kila inapoitwa leo, kila siku linagundulika jambo jipya halikadhalika na vitu vipya.

Ukiwa Msichana Mjinga utataka ukimbizane na kila aina ya mitindo ya mavazi na maisha yanayoibuka kila leo. Na kwa kufanya hivi bila shaka utapoteza muelekeo wa maisha yako. Ni vizuri kwenda na wakati ila inahuzunisha ikiwa wakati utakupelekesha kwenye kila jambo.

Na kiukweli sio kila jambo linaloibuka jipya iwe mtindo au chochote litakufaa ama ni lazima ukimbizane nalo. Kuna mengine yaache tu yapite mbali nawe, mengine yaache yaende, na mengine yaone tu kwa

wengine. Isipokuwa yale ambayo yanaendana na NDOTO/ MAONO yako kwa faida, komaa nayo.

Mara nyingi Wasichana wengi wajinga, hukimbizana na mitindo mipya ili kujitafutia umaarufu, yaani ajulikane na kila mtu na ajione yeye ni bora na wa thamani kuliko wengine. Huku ndiko kunaitwa kutaka UMAARUFU.

Mithali 3:30 ***"Usishindane na mtu bila sababu, Ikiwa hakukudhuru kwa lo lote."***

Wasichokijua wengi UMAARUFU una gharama na hasara kubwa kuliko faida. Na ni heri UMAARUFU unaokujia wenyewe kuliko ule wa kuutafuta. Umaarufu una tabia ya kukuondolea uhuru binafsi. Na ukikaa vibaya baada ya muda umaarufu ni fedheha.

Ushauri wangu ni ACHA MASHINDANO yasiyo na maana, ACHA KUJITUTUMUA kwa mambo usiyo na uwezo nayo. Kama ni kutambulika ACHA BWANA atakutambulisha mwenyewe, kama ni kuinuliwa ACHA BWANA Akuinue mwenyewe. Biblia inasema MUNGU humwinua mnyonge kutoka mavumbini na kumketisha pamoja na Wakuu. Na ni Heri kuinuliwa na BWANA kuliko kuwatumainia wanadamu.

Mungu akupe HEKIMA Msichana, ya kukabili changamoto za Mitindo na Umaarufu katika Jina la Yesu!.

# MPAKA LEO HAJUI KWAMBA SHULE SIO LAZIMA KUAJIRIWA.

Ukiwachukua Wasichana Saba leo wanaosoma aidha sekondari au chuo, na ukiwauliza kwanini wanasoma wanachosoma kwa bidii? Sita kati yao watakwambia wanasoma ili wafaulu vizuri KISHA waajiriwe, wawe na kazi na mshahara mzuri, na hatimaye maisha mazuri. Ni msichana asiye mjinga tu anayeelewa kwamba kwa dunia ya leo suala la AJIRA ( kuajiriwa ) limekuwa fumbo na kitendawili kisichoteguliwa kwa urahisi. Ule msemo wa SOMA MWANANGU UAJIRIWE karibu unakwenda kupitwa na wakati na kupotea jumla.

Nimewaona Wasichana wengi waliopoteza MWELEKEO na TUMAINI la maisha mara baada ya kumaliza vyuo na kusota mtaani. Na ndio maana kwa dunia ya leo nimehesabu kuwa ni ujinga ikiwa kuna msichana anayesoma akiwaza kuajiriwa peke yake. Na tatizo la ukosefu wa ajira ni tatizo la kidunia, wala si la Tanzania peke yake. Hekima inatutaka kuona hatari mbele na kuanza kuikabili mapema kabla hatujaifikia.

Kusoma kuzuri sana, ni muhimu na kunapendeza. Ajira nayo sio jambo baya kiukweli, huko nyuma ajira zilikuwa nyingi na wazi sana, kwa maana wasomi walikuwa wachache na mahitaji yalikuwa makubwa sana. Lakini leo kila familia ina kijana aidha mwenye shahada au walau stashahada. Kwa mwaka maelfu ya vijana wanahitimu vyuo

vikuu katika kada mbalimbali. Na wanaostaafu ni wachache NA mahitaji serikalini na kwenye sekta binafsi ni madogo sana. Kwa sababu hii ni lazima ushtuke mapema na uchukue hatua. Ni muhimu ujiandae kifikra, kimtazamo na kivitendo ili kukabiliana na hali ya ukosefu wa ajira. Soma kwa bidii na kwa kiwango unachotaka ILA jiandae kujitengenezea ajira yako binafsi, hii inaitwa KUJIAJIRI.

Mtaani kuna fursa kibao na uhitaji ni mwingi sana, Mtaji na Rasilimali tayari ni wewe mwenyewe. Kikubwa tambua unahitaji kuja na WAZO litakalokutoa kimaisha kwa kuwa suluhisho la hitaji/ tatizo flani miongoni mwa jamii. Kumbuka sio lazima utakachokifanya kiendane na ulichosomea/ unachosomea kwani **Kwa mfano** kuna msomi wa shahada flani

alivyohitimu alikuja mtaani na kuanza kuuza UJI, mwingine MATUNDA, mwingine JUISI, mwingine amekuwa MKULIMA hodari, mwingine MUONGOZAJI SHEREHE (MC) na mwingine huduma za UDOBI mtaani. NA wengine wakaweka shahada zao mfukoni na kuamua kutumia VIPAJI vyao kutengeneza pesa mtaani. Kwa taarifa yako mambo ya kufanya ni mengi kuliko unavyofikiria, suala ni uamue kuanza KUONA.

Nimesema nikuondoe huu UJINGA bhana, usije kusema LAITI ningelijua. Kakako nimeona nikwambie mapema, usije ukasota mtaani huku ukilaumu serikali, dada zako wengi walitamani wangeyafahamu haya mapema ila ndio hivyo.

.

# ANADHANI WAZAZI WAMEPITWA NA WAKATI !

Moja kati ya tabia mbaya na za ajabu sana nilizoziona kwa Msichana Mjinga ni kudharau wazazi wake na kudhania wamepitwa na wakati. Wasichana wengi wa leo hasa ambao wameenda shule kidogo hata ambao wamepata kafursa cha kuishi mijini, wamekuwa na tabia ya kuwadharau, kutowasikiliza na kuwachukulia poa wazazi.

Mithali 30:17 ***"Jicho la mtu amdhihakiye babaye, Na kudharau kumtii mamaye; Kunguru wa bondeni wataling'oa, Na vifaranga wa tai watalila. "***

Maandiko Matakatifu yanasema kwa uwazi sana ya kwamba mtu wa aina hii hawezi kubaki salama,wengi wao wanakosa baraka na hatimaye wanakosa muelekeo mzuri kimaisha.

Yapo mambo mengi sana ambayo wazazi wamekuwa wakiwaonya, wakiyakemea, wakiyakosoa na kuwaelekeza watoto wao wa kike, lakini wengi wao wamekuwa wakiyadharau na kuyapuuza. Nisikilize binti, haijalishi umesoma, umeumbika au una ujanja wa kiasi gani, Wazazi au Walezi wako wanayajua maisha na dunia kuliko wewe kwa taarifa yako. Ndio maana Mungu akasema ;

Waefeso 6:2,3 *"**Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi, Upate heri, ukae siku nyingi katika dunia.** "*

Ukifanikiwa kutia bidii katika kuwaheshimu wazazi wako, Neno la Mungu linasema ya kwamba nyuma yake kuna ahadi toka kwa Mungu ya kubarikiwa na kuongezewa siku za kuishi hapa duniani.

Msichana Mjinga hajui AHADI inayoambatana na kuwaheshimu wazazi wake, yaani hapa haijalishi wazazi wamesoma au hawajasoma, wanajua au hawajui, ni maskini au matajiri. Ishu hapa ni kwamba JIFUNZE na tia bidii kuwasikiliza, kuwaheshimu na kuwathamini wazazi wako. Ukielekezwa jambo na Baba au Mama au Mlezi wako, Weka umakini mkubwa katika hilo. Msichana mjinga hudhani kwamba labda kwa sababu amesoma kuliko wazazi wake, basi kila analofanya yuko sahihi. Maandiko yanasema hivi;

Mithali 14:12 ***"Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, Lakini mwisho wake ni njia za mauti.*** *"*

Na ndio maana, licha ya wasichana wengi kusoma vizuri na kufaulu masomo shuleni

au vyuoni bado wana ujinga mwingi tu. Unakuta msichana kimuonekano na kielimu yupo vizuri sana, ila bado anakwama kwenye mambo mengi sana. Matokeo yake wengi wanaishia kuchezewa, wengi wanaishia kuhangaika na maisha, na zaidi wengi wanafanya mambo mengi yasiyofaa. Ipo siri kubwa na ahadi ya ki Mungu katika kuwaheshimu wazazi wako, wanaweza wasiwe sahihi kwenye kila jambo ILA jifunze kuwatii kwa hekima wasijisikie vibaya. Mara zote wazazi wetu hufanya mambo ili kututakia mema.

Nakuombea wewe uliyekengeuka ambaye husikii la Mama wala Baba, Mungu akurejeshe katika heshima na adabu kwa wazazi wako. Na kama uliwakosea heshima, rudi nyumbani waangukie waambie wazazi wangu nimekosa naomba mnisamehe.

Mithali 4:3 "***Maana nalikuwa mwana kwa baba yangu, Mpole, mpenzi wa pekee wa mama yangu.*** "

Ninajua pia wapo ambao walikosewa na wazazi wao kwa namna moja au nyingine, tafadhali naomba sikiliza kwa umakini sana. Chukua hatua, fungua moyo wako na wasamehe kabisa, sahau kila jambo baya walilokukosea na ANZA NAO UPYA. Zipo baraka, Ipo ahadi, Kuna furaha na Amani isiyo ya kawaida katika mahusiano bora na mazuri na wazazi wako.

Msichana eeh, tambua leo kwamba Mungu ndiye alitaka, na aliwaamini hao wazazi wako kukuleta duniani. Hauna cha kubadili ili hao wasiwe wazazi wako, unao uchaguzi mmoja tu wa kuwakubali, kuwapenda, kuwaheshimu na kuwashukuru ili upate

Heri na siku nyingi za kuishi duniani. UCHAGUZI NI WAKO.

Aliyetangulia Katangulia. Na sikiliza, hakuna aliyewahi kuwadharau wazazi wake na AKABAKI SALAMA. Pona huo UJINGA katika Jina la Yesu.

## ANAAMINI ZAWADI NA MAWASILIANO NDIO ISHARA TOSHELEVU YA UPENDO.

Naomba nianze na kauli hii muhimu sana ***"HAUWEZI KUPENDA bila KUTOA, ila sio kila KUTOA ni ISHARA YA UPENDO."*** Kama kila msichana angeielewa hii kauli na ikamwingia akilini na akaifanyia kazi, basi tungekuwa na Wasichana wachache sana ambao wangedanganyika.

Lakini cha kustaajabisha leo tuna maelfu ya mabinti ambao unapojaribu kuwauliza kwa nini wanaamini kwamba wanaume walionao kwenye mahusiano wanawapenda, watakachokujibu ni kwa kuwa ananijali, ananipa kila ninachokitaka na haachi kuwasiliana na mimi. Wasichojua kuhusu haya ni hiki hapa, sio kila KUTOA na sio kila KUWASILIANA ni ishara toshelevu ya UPENDO.

1 Wakorintho 13:3 ***"Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidii kitu."***

Maandiko yanaonyesha kwamba UPENDO ni zaidi ya KUTOA, na kwa maana rahisi ni kwamba mtu anaweza KUTOA bila UPENDO. Mara nyingi ndani ya UPENDO kuna msukumo wa KUTOA, lakini hiyo haimaanishi kila KUTOA maana yake ni KUPENDA. Na nikutoe ujinga leo, moja kati ya tabia za UPENDO ni, UPENDO hautafuti mambo yake au hauangalii matakwa yake. Sasa sikiliza mvulana / mwanaume yeyote anayekutamani, daima atakuwa tayari kukupa chochote kulingana na uwezo wake ili tu akushawishi APATE ANACHOKITAKA kwako ( mwili wako ). Atakubembeleza, Atakujali, Atakudekeza,

Atakutafuta kila wakati kukujulia hali, atakununulia chochote nasema tena chochote ili tu APATE MWILI WAKO na atimize tamaa zake. Na ndio maana wengi wa wasichana mara tu baada ya kutoa miili yao sadaka kwa wanaume wanaodhania kwamba wanawapenda, ghafla mawasiliano na zawadi zikaanza kupungua na hatimaye zikaisha kabisa.

Usiendelee kujidanganya na vizawadi hivyo wala mawasiliano ya mara kwa mara. Hivi havitoshi kupima UPENDO WA KWELI, kuna mambo muhimu zaidi ya hayo ambayo tunaweza kuhesabu kama viashiria vya UPENDO wa KWELI. Kwa mfano, Mwanaume ambaye anajali na anaheshimu MAHUSIANO yako na Mungu yaani hakusukumi kwenye DHAMBI, MWANAUME anayeheshimu NDOTO,

MISIMAMO na MIPAKA uliyomuwekea, MWANAUME ambaye yuko tayari kukusubiri na kusubiri muda sahihi wa tukio sahihi. MWANAUME anayekukemea na kukurekebisha unapokosea, MWANAUME anayetaka kukuona unakuwa salama kila wakati. MWANAUME anayejali na anayethamini MAMBO YAKO, MWANAUME mwenye malengo na ratiba zinazoeleweka na wewe TENA asiyejivuna. Sauti INATOSHA?

## HAJUI HARUSI NI TUKIO NA NDOA NI AGANO.

Kwenye fikra za Wasichana wengi leo unapowauliza kuhusu KUOLEWA, utashangaa wengi wao wanavyoelezea vile watakavyovaa magauni mazuri na ya kisasa tena ya gharama kubwa katika sherehe zao za kitchen party, Sendoff na Harusi. Utashangaa zaidi anapoanza kuelezea muonekano wake na namna atakavyoingia ukumbini, namna atakavyotoa kisauti flani amaizing kanisani kwenye ahadi ya ndoa, vile atakavyopokea mizawadi ukumbini NA namna atamtambulisha Hubby wake.

Mwisho wa siku unakuja kugundua kwamba wengi ni wajinga, na ndio maana wanajiandaa zaidi na HARUSI kuliko NDOA.

***Mwanzo 2:24 "Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye***

***ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja. "***

Harusi ni sherehe na tukio la siku moja, lakini Ndoa ni Agano la Kuishi na mumeo mpaka kifo kitakapowatenganisha. Na ndio maana Wasichana wengi wanafanikiwa sana kwenye harusi, na wanafeli sana kwenye Ndoa. Unajua ni kwa nini? Ni kwa sababu waliweka nguvu kubwa kwenye maandalizi kwa ajili ya Harusi na kudharau maandalizi ya Ndoa. Wengi hata leo wanajua sana kuhusu Harusi ila hawajui kabisa kuhusu Ndoa.

Ni muhimu uanze sasa kudhamiria kuondoka kwenye kundi la wasichana wajinga wanaowekeza nguvu kwa ajili ya Harusi badala ya Ndoa. Unajua baada ya Tukio yaani HARUSI, kinachobaki na kudumu ni Agano yaani NDOA. Msichana

mwenye hekima huanza kujifunza kwa bidii kuhusu NDOA kabla ya kuamua kuingia kwenye ndoa. Ni vizuri uelewe kwa kina nini maana ya NDOA , nini maana ya KUOLEWA, pia ujue MKE ni mtu wa aina gani. Yaani uelewe MAANA, NAFASI, MAJUKUMU na WAJIBU wa kuwa MKE wa mtu, na MAMA wa Watoto.

Wengi ambao hawakuchukua muda na nafasi ya kujifunza haya, wamekuwa mizigo na kikwazo kwenye NDOA zao. Waliolewa kwa mbwembwe na bashasha, ila sasa wamepoa wanatamani siku zirudi nyuma. Ninakuombea Neema ya Mungu na Akili nzuri ili uwe tayari KUJIFUNZA kwa kusoma vitabu sahihi vinavyohusu NDOA, pata nafasi ya kujifunza kwa kuuliza waliotangulia na angalau wamefanikiwa kwenye NDOA, hudhuria mafundisho na

semina za maandalizi ya Ndoa za Kikristo, soma NENO LA MUNGU, na usiache KUOMBA ili Mungu akupe Neema ya kuwa MKE MWEMA na kukupa MUME MWEMA.

NDOA sio mbwembwe za HARUSi, NDOA ni zaidi ya harusi, NDOA ni zaidi ya KUOLEWA, NDOA ni zaidi ya TENDO LA NDOA, NDOA ni zaidi ya kuzaa WATOTO.

**Wekeza kwenye NDOA na sio HARUSI peke yake.**

# HAJUI MWANAUME NI KAMA MICROWAVE!

Daima nimekuwa nikiwaambia Wasichana kila mahali ninapokutana nao kwamba TRUST NO MAN 100% yaani USIMUAMINI MWANAUME YEYOTE kwa 100%. Na huwa nawasisitiza hivi hata kama ni Baba yako mzazi, hata kama ni nabii wako, Mjomba wako, sijui nani wako, ACHA KABISA, badala yake JIHAMI kila wakati na faragha na mazingira yasiyoeleweka yaani mazingira hatarishi.

Sisemi haya kwa kukurupuka, ninayo mifano na shuhuda za kutosha, kwa miaka hii zaidi ya 11 ambayo nimekuwa nikiwahudumia mabinti na vijana.Ninazo shuhuda za mabinti waliojikuta wamebakwa au kulazimishwa au kutishwa au kushawishiwa na Baba zao wa kuwazaa,

Wachungaji wao na orodha inaendelea na kuendelea.

Sikilizeni Wasichana, tena sikilizeni kwa makini sana. Ninajua wengi wenu mmeshawahi kutumia, kuona ama kusikia kile kifaa kinachotumika kupasha chakula kwa haraka sana kinachoitwa MICROWAVE kwa lugha ya kigeni. Basi moja ya tabia ya kile kifaa ni kupasha moto kwa haraka sana unapowasha tu, na pia ni kukata moto kwa haraka sana unapozima tu. Sasa halikadhalika tamaa ya ngono kwa wanaume, huwa inawaka kwa haraka sana kulingana na mazingira bila kujali sana ni nani na nini kitatokea baada ya hapo. Matamanio ya tendo hili (SEX ) kwa wanaume lina nguvu isiyoweza elezeka kwa urahisi, na ndio maana Daudi alipomuona mke wa Huria anaoga alishindwa kujizuia,

na Yusufu alipotaka kulazimishwa na mke wa Potifa alikimbia.

Sikiliza Binti, unaweza kujikuta unafanya au unafanyiwa jambo la ajabu sana na mtu usiyetegemea na uliyemuamini kupitiliza kisa tu tayari anaitwa MWANAUME. Wengi wa Wanaume ile tamaa ikiwashika hasa kwa mazingira uliyomtengenezea au mliyotengeneza kwa pamoja huwa hajali nini kitatokea atataka tu amalize tamaa yake kwanza.

Sehemu kubwa ya ubongo wa mwanaume inawaza tendo hilo (SEX ), Epuka sana kuvaa mavazi yanayoonyesha maumbile yako na jiweke mbali na mazingira hatarishi kwako. Usije kusema Bro hakuniambia, maana ndio nakuambia sasa. Ila kama unataka mwenyewe sasa hiyo ni juu yako ila kumbuka MAJUTO NI MJUKUU.

Mnakumbuka nilisema kwamba MICROWAVE huwa inakata moto haraka pia?, ndio maana mwanaume akimalizana na wewe anakuwa kama hakutaki wala havutiwi tena na wewe kivile, na isitoshe anaanza kujuta ama kukulaumu na mwingine anakufukuza kabisa. Na wengi wenu hii imewaumiza sana.

**NISIKILIZE tena TRUST NO MAN 100%, EPUKA MAZINGIRA HATARISHI!**

# HAJUI KWA MWANAUME NGONO NA UPENDO HAVIHUSIANI.

Kwa Mwanaume NGONO ni NGONO, na UPENDO ni UPENDO, yaani hakuna mwingiliano wala mahusiano. Niwarahisishie zaidi, yaani ni hivi MWANAUME anaweza kufanya NGONO na msichana yeyote mahali popote na sio lazima awe amempenda.

Yaani usijidanganye eti kwa kuwa anakutaka ndio anakupenda, shauri yako na ujinga wako. Mwanaume anaweza kuvutiwa na rangi yako, na muonekano wako na akakutaka kingono tu na si vinginevyo.

Najua inakuwa ngumu kidogo kunielewa kwakuwa kwa mwanamke NGONO na UPENDO vinahusiana kwa karibu sana. Achilia mbali wale wanaofanyia biashara miili yao, hakuna msichana yupo tayari kulala na mwanaume asiyempenda. Kwa mwanamke Upendo na Ngono vinaendana bega kwa bega yaani ni mapacha. Na ndio maana akili zenu huwa zinafikiri na kwa mwanaume ni hivyo hivyo pia. Hii ndio sababu wengi wa mabinti huwa wanaishia kuumia, kwa sababu yeye alifanya kwa kupenda kumbe kwa mwanaume ilikuwa ni suala la kumaliza tamaa zake. Weka akilini hiyo, na ujinga ukutoke.

Na wale ambao huwa mnajidanganya kwa kudanganywa pia na wanaume kwamba eti ukimpa PENZI ndio atakupenda zaidi, naamini mmeshapata majibu yenu kamili.

Yaani hata kama ungemfanyia nini kitandani, kama hakupendi atakupa tu maneno ya danganya toto ya kukutia moyo. Na atakuwa anakukumbuka na anakutafuta anapopata tamaa ya Ngono. Kwa maana nyingine kwake unakuwa kama KIFAA CHA STAREHE tu.

Na ndio maana sio sahihi kujilengesha mwili wako kwa mwanaume ili akupende AMA wengine wanajibebesha na mimba kabisa eti ili waolewe. Mwisho wa siku wengi wanakula hasara, na matokeo yake wanalea watoto kwa tabu kubwa sana. Tulizana na Mwamini Mungu, Wewe ni wa thamani, Mwili wako ni Hekalu la Roho Mtakatifu, Kesho yako imehakikishwa na Mungu mwenyewe, ACHA PAPARA.

Acha tu niishie hapa, kuna ambao wanaumia na UKWELI huu, Acha nisichome hii sindano zaidi.

## ANAAMINI HAWEZI KUISHI BILA MTU FULANI.

Ushasikiaga wale mabinti wa SIWEZI KUISHI BILA WEWE au wale wa BILA YA WEWE MAISHA YANGU HAYANA MAANA au wale wa BILA WEWE BORA NIFE. Achana sasa na wale wa Wewe ni KAMA HEWA NINAYOVUTA, MAJI NINAYOKUNYWA na CHAKULA ninachokula. Yaani bila huyo mtu hakuna UHAI na of course HAKUNA MAISHA.

Nimewahi kusikia kuna ambao walipopigwa kibuti WALIKUNYWA SUMU wakawahiwa na maziwa, na kuna wengine waliojiachia gorofani na sasa hawana

miguu. Na wapo ambao waliacha vyuo, wengine waliachia mitihani katikati, na wengine wakanywa mikojo yao wakijiapisha HAWATAPENDA tena. Kila mmoja just kulingana na kiwango cha UJINGA na UPUMBAVU wake.

**Yeremia 17:7,5 " Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea BWANA, Ambaye BWANA ni tumaini lake. BWANA asema hivi, Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, Amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake Na moyoni amemwacha BWANA. "**

Kama kuna ujinga duniani ni KUMPENDA mtu kuliko UNAVYOJIPENDA wewe, Biblia inasema MPENDE jirani yako kama nafsi yako. Kuharibu maisha yako sababu ya mtu mwingine ni kiwango cha juu sana cha UJINGA. Kuna mabinti wanadhania

kwamba MAPENZI yalianzia kwao, bila kufahamu kwamba yalianzia bustani ya Edeni. Ujinga zaidi ni kuweka TUMAINI / IMANI yako kwa mwanadamu anayebadilika ndani ya sehemu ya sekunde KULIKO Mungu asiyebadilika ambaye Yeye ni Yeye yule JANA, LEO na hata MILELE na amesema hana kigeugeu.

Wengi wenu mnaumizwa na mapenzi na mahusiano maana mmeweka tumaini na imani kwa wanaume kuliko kwa Mungu. Mnawatii na kuwasikiliza sana boyfriends zenu kuliko kumtii na kumsikiliza Mungu. Na ndio maana siku mkiachwa mnawaza kufa tu, unajua ni kwa nini AMELAANIWA mtu anayemtegemea mwanadamu. Laana inawala ahahahaha BADILIKENI.

Zipo faida, Zipo baraka, Ipo amani, Ipo furaha, Upo utulivu kwenye kumtegemea na

kumtumaini Mungu. Ondokana na usumbufu, msongo wa mawazo, maumivu na kuchanganyikiwa kwa kumkabidhi Yesu maisha yako na kumuamini ya kwamba Yeye ni kiongozi wa MAISHA yako.

Mapenzi ya kweli na matamu yanapatikana ndani ya YESU, Mume mwema na mwaminifu anapatikana kwa YESU. Anakuita leo kwa upole, Anakuita sasa AKUPUMZISHE na vibuti, usaliti na utumwa wa MAPENZI na NGONO NJOO KWAKE SASA!.

# OMBA NA MIMI MAOMBI HAYA;

Ikiwa Umekisoma Kitabu hiki, na kuna namna ambayo umegundua haukuwa sahihi NA Ungelipenda leo kumkabidhi Yesu Maisha yako ili awe BWANA na MWOKOZI wako, Omba SALA hii pamoja nami;

**EEH MUNGU BABA KATIKA JINA LA YESU, NIMEUONA WEMA WAKO NA MKONO WAKO KUPITIA MAFUNDISHO YA KITABU HIKI.**

**"Mimi...............................................NI MEAMUA KUKUPOKEA YESU UWE BWANA NA MWOKOZI WA MAISHA YANGU. NINATUBU DHAMBI**

**ZANGU ZOTE NILIZOTENDA MBELE YAKO KWA DAMU YA YESU!. NINAKUPOKEA YESU MAISHANI MWANGU KUANZIA SASA NA HATA MILELE. ROHO MTAKATIFU KARIBU MAISHANI MWANGU, NIONGOZE NA NIFUNDISHE KATIKA KWELI YOTE, AMINA."**

Ikiwa umeomba Maombi haya pamoja nami, nichukue nafasi hii kipekee kukuomba utujuze yale ambayo Mungu ametenda kwako kwa 0752307008 / 0715307008.

**HONGERA KWA KUOKOKA!.**